United Nations
Educational, Scientific and
Cultural Organization

Viongozi wa Kimila:

FAHAMU ZAIDI kuhusu CSE na Huduma Rafiki kwa Vijana!

Mustakabali unaofaa, na wenye tija kwa vijana!

Elimu ya kina ya ujinsia, afya ya uzazi, maadili ya afya na stadi za maisha (CSE) ni taarifa ya kiutamaduni na inayofaa kutolewa kulingana na umri ambayo inawafundisha vijana kuhusu masuala ya ujinsia na ngono na afya ya uzazi.

Ushahidi unaonyesha kwamba CSE inaongeza ufahamu wa watoto kuhusu VVU, inawasaidia kuchelewa kufanya ngono, kupunguza idadi ya wenzi ngono walionao na kuongeza uelewa wao na matumizi ya kingamimba pale wanapohitaji kuzuia uambukizo kwa ngono (STIs) na VVU, pamoja na mimba za utotoni.

Unga mkono CSE - Saidia viongozi wetu wa baadaye!

Kwa nini CSE na Huduma rafiki kwa Vijana Vinakwenda Pamoja

Elimu ya ujinsia inahitaji kuungwa mkono kwa taarifa na huduma za afya kupatikana, kuweza kumudiwa na kutolewa kwa ufanisi. Vijana na jamii zao wanabakia katika hatari bila ya bidhaa zinazoweza kuwasaidia, ikiwemo: kondomu, kingamimba za kisasa, matibabu ya VVU na maambukizo kwa ngono, ushauri wa mimba na matunzo na huduma nyingine. Hii ndiyo maana kujumuisha CSE katika shule na huduma rafiki kwa vijana katika jamii ni njia ya kuimarisha afya kwa muda mrefu katika nchi za mashariki na kusini mwa Afrika.

Huduma Rafiki Ya Ngono na Afya ya Uzazi kwa Vijana ni Nini (YFS)?

Huduma rafiki za ngono na afya ya uzazi kwa vijana (YFS) zinatoa huduma za afya zinazolenga uelewa wa kina wa nini ambacho vijana katika jamii yoyote ile au jumuiya wanataka na kukihitaji. Zinahusisha afya ya uzazi ya vijana, haki na utofauti.

YFS zinajumuisha:

- Unasihi kuhusu ujinsia na afya ya uzazi.
- Unasihi kuhusu uhusiano na ujinsia.
- Unasihi kuhusu unyanyasaji wa kingono.
- Unasihi kuhusu kingamimba na utoaji wa kingamimba, ikiwemo kinga mimba ya dharura.
- Kuzuia uambukizo kwa ngono (vikiwemo VVU), huduma za upimaji na unasihi.
- Huduma za kutoa mimba (pale ambapo inaruhusiwa kisheria).
- Huduma za kabla na baada ya kujifungua.

Ujinsia na afya ya uzazi (SRH) ni elimu, ujuzi na uwezo wa kufanya uchaguzi unaofaa, mzuri, na unaotolewa baada ya kuwa na taarifa za mapema na za kutosha na kufanya uchaguzi salama wa ngono - ikiwa ni pamoja na KUTOFANYA ngono.

Kwa nini viongozi wa kimila wanapaswa kuhusishwa na kusaidia CSE?

Baadhi ya watu wanahisi kwamba kuzungumza na watoto kuhusu elimu ya ujinsia shuleni au katika vyanzo vilivyopo nje ya familia au kwenye mtandao wa kijamii ni kinyume cha mila na utamaduni. Kwa wengi ni mwiko kuzungumzia masuala yanayohusu ujinsia, uhusiano na SRH na watoto na vijana.

"Asiyesikia la mkuu huvunjika guu."

—Methali ya Kiafrika

Siku hizi, watoto watapata taarifa hizi kutoka katika vyanzo vingine vingi ambavyo si wakati wote huwasaidia (televisheni, redio, simu za mkononi, magazeti n.k.) Hata familia zinabadilika na vyanzo vya kimila havipo hapo wakati wote kwa ajili ya watoto wote. Kwa kuwa na maambukizo ya kiwango cha juu ya VVU miongoni mwa wenye umri wa miaka kati ya 15 - 24, kunaonyesha kukosekana kwa vyanzo vinavyofaa vya taarifa na hivyo kusababisha madhara makubwa.

"Busara ni kama mbuyu; hakuna yeyote anayeweza kuukumbatia."

—Methali ya Akan

Kutowahusisha watoto na vijana katika majadiliano yanayohusu ujinsia na afya ya uzazi kunawaweka katika uwezekano wa kuambukizwa VVU na Magonjwa Yanayoambukizwa kwa Ngono (STI) pamoja na mimba zisizotarajiwa na za mapema, kukeketwa, ukatili na unyanyasaji wa kingono. Viongozi wa kimila wanaweza kusaidia kuvunja miiko hiyo.

Wajibu wangu ni nini kama Kiongozi wa Kimila?

"Maarifa bila busara ni kama maji katika mchanga"

—Methali ya Guinea

Zungumza: Kama kiongozi wa kimila, unaweza kuongoza njia na kuwahamasisha wengine kuzungumza na vijana kuhusu masuala haya muhimu ya afya. Watu wanatafuta kwako mwongozo na uongozi kuhusiana na jinsi CSE na YFS zinazofundishwa shuleni na katika jamii zinavyoendana na taratibu za kitamaduni na kimila na miiko.

Yajue Masuala haya: Mmoja kati ya watu watatu katika nchi za mashariki na kusini mwa Afrika ana umri wa miaka 10-24 na chini ya 40% kati yao wana taarifa za kutosha kuhusu VVU. Vijana hamsini na mbili wanaambukizwa VVU kila saa.

Saidia upataji taarifa, matibabu na matunzo kwa vijana: CSE katika shule na YFS katika jamii sio tu kwa ajili ya vijana amilifu kingono. Ni unyanyapaa huu ambao unawaweka hatarini vijana wanaohitaji taarifa. Taarifa sahihi zinazotoka moja kwa moja kwa watoa huduma za afya zinaweza kuwa na matokeo mazuri sana katika kuendeleza mwenendo mzuri wa afya ya vijana.

Viongozi wanawalinda wote: Ni wajibu wako kuhakikisha kwamba haki zote za watoto na vijana zinadumishwa ili waweze kufanya uamuzi wakiwa na taarifa za kutosha na kufanya uamuzi wa uwajibikaji na kuishi maisha mazuri, yenye tija na ya ukamilifu. Vijana ni taifa letu la kesho; wasaidie!

"Watoto ni zawadi ya maisha."

— Methali ya Kiafrika

Nifanye nini kusaidia, nikiwa kama kiongozi wa Kimila?

- ***Bainisha kwamba CSE na YFS inaendeleza ujizuiaji katika kufanya ngono kama mbinu ya msingi na yenye ufanisi zaidi ya ngono salama.*** Hatahivyo,bila kuwa na taarifa kuhusu njia nyingine, jitihada za kuhamasisha afya, tabia ya uwajibikaji kwa watoto na vijana zina ufanisi mdogo.
- ***Saidia klabu za CSE na YFS katika jamii.*** Shirikiana na shule na watoa huduma kuanzisha mazingira yasiyokuwa na unyanyapaa wala ubaguzi wakati vijana wanapochagua kuwa salama.
- ***Mazungumzo ya kiutamaduni:*** Shiriki katika mazungumzo ya kiutamaduni na kuhamasisha vitendo chanya ambavyo vinalinda haki za watoto na vijana.
- ***Vunja ukimya:*** Zungumza wazi dhidi ya taratibu za kiutamaduni zenye madhara, ikiwemo: matambiko ya kimila yasiyo salama, uhusiano wa kingono wa watu wa rika tofauti kati ya watoto na watu wazima, ndoa za utotoni, ndoa za kulazimishwa, mimba za utotoni, kurithi mke na unyanyapaa kwa watu wanaoishi na VVU, ulemavu na tofauti nyingine.

Watoto na Vijana Waliopewa taarifa za kutosha:
Uchaguzi wenye taarifa za Kutosha - Unaweza Kuongoza Njia!

United Nations Educational, Scientific and Cultural Organization
SWEDEN
Norad
SAfAIDS
Knowledge for action: The power to make a difference!

Ofisi ya Kanda ya SAfAIDS, Zimbabwe:
Barabara ya 17 Beveridge, Avondale, S.L.P A509, Avondale, Harare, Zimbabwe
Simu: +263 4 336 193/4, Faksi: +263 4 336 195
Tovuti: www.safaids.net